

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA IRINGA**  
*(Barua zote zielekezwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa)*

Simu Na. 026 - 2702647  
Faksi Na. 026 – 2702203  
Email:mkurugenzi@iringamc.go.tz



Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa,  
S.L.P 162,  
**IRINGA.**

**7/05/2018**

**TANGAZO LA ZABUNI YA UWAKALA WA USHURU KWA  
MWAKA WA FEDHA 2018/2019**

1. Halmashauri ya Manispaa ya Iringa katika mwaka wa fedha 2018/2019 inakusudia kukusanya mapato katika vianzia vyake mbalimbali kwa mkataba wa mwaka mmoja kuanzia tarehe 1/07/2018 mpaka 30/06/2019. Halmashauri ya Manispaa ya Iringa inawatangazia Wananchi, Makampuni, Taasisi mbalimbali na vikundi vilivyoandikishwa kuleta maombi ya Zabuni za uwakala wa ushuru kama ifuatavyo:-

<b>Na</b>	<b>NAMBA YA ZABUNI</b>	<b>JINA LA ZABUNI</b>	<b>ADA YA MAOMBI</b>
1	LGA/025/2017/2018/NC/01	MAENEO YOTE YANAYOEGESHWA MAGARI NDANI YA MANISPAA YA IRINGA.	100,000/=
2	LGA/025/2017/2018/NC/02	USHURU WA VITUO VYA STADI KUU, IPOGOLO, MLANDEGE NA MIYOMBONI	100,000/=
3	LGA/025/2017/2018/NC/03	HUDUMA YA VYOO (STENDI KUU, SOKO KUU, KIHESA, KITWIRU NA IPOGOLO)	100,000/=

2. Mchakato wa Zabuni hizi utaedeshwa chini ya utaratibu wa Zabuni za ushindani kwa waombaji wenyeji (Preference to Local Communities) kama inavyoelekezwa kwenye Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013- Tangazo la Serikali No. 446 na Zabuni ziko

wazi kwa waombaji wote wenyeji au vinginevyo kama itakavyoelezwa kwenye Nyaraka ya Zabuni, Sehemu ya vigezo vya maandalizi ya zabuni (Tender data sheet).

3. Waombaji wenye nia na sifa wanaweza kupata ufafanuzi zaidi kwa kununua na kusoma nyaraka ya Zabuni katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Maispaa S.L.P 162, IRINGA, kuanzia saa 2.30 asubuhi hadi saa 9.30 Jioni siku za Jumatatu hadi Ijumaa isipokuwa kwa siku za sikukuu.
4. Seti nzima ya nyaraka za zabuni zikiwa katika lugha ya Kiswahili zianaweza kununuliwa na Wazabuni wenye nia kwa kuleta maombi kimaandishi kwa anuani iliyotajwa katika aya ya tatu hapo juu kwa malipo ya Tshs. 100,000.00 ambazo hazitarudishwa hata kama mwombaji hatashinda Zabuni. Malipo yafanyike kwa hundi au kupitia benki kwa Mkurugenzi wa Manispaa.
5. Zabuni zote ziambatane na kiapo cha dhamana ya Zabuni (Tender securing declaration) kwa kuzingatia fomati iliyoainishwa katika kabrusha la Zabuni.
6. Zabuni zote zitumwe katika nakala moja halisi na nakala mbili vivuli zikiwa zimefungwa vizuri kwa lakiri kwenye bahasha bila kuwa na alama yoyote inayoashiria zilikutoka na zitumwe kwa:-

**MKURUGENZI  
HALMASHAURI YA MANISPAA,  
S.L.P 162,  
IRINGA.**

7. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 22.05.2018 saa nne kamili asubuhi na Zabuni zitafunguliwa hadharani mara tu baada ya siku na saa hiyo kuwadia kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri ya Manispaa ya Iringa. Waombaji au Wawakilishi wao wanaalikwa kwenye zoezi la ufunguzi iwapo watahiari.
8. Zabuni ambazo hazitapokelewa na kusomwa hadharani siku ya ufunguzi wa Zabuni hazitafikiriwa na Taasisi nunuzi hata kwa sababu yeyote ile.
9. Halmashauri ya Manispaa ya Iringa hailazimiki kukubali kiwango cha marejesho na kamisheni cha chini au cha juu.

**MKURUGENZI WA MANISPAA  
IRINGA**